



KISHINDO CHA SAMIA

BAHI | IKUNGI | MANYONI | SINGIDA





RAIS SAMIA KUJENGA BANDARI KAVU NA KITUO CHA SGR BAHİ

Mgombea urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Dkt Samia Suluhu Hassan amesema akipata ridhaa ya kuongoza kupindi kingine atajenga bandari kavu na Kituo cha Treni ya Mwendokasi (SGR) wilaya ya Bahi.

Rais Samia ameyasema hayo leo asubuhi wilayani humo wakati akihutubia wafuasi wa Chama hicho waliokusanyika kumsikiliza akinadi sera zake.

“Vituo hivi vitavutia uwekezaji na biashara na Bahi itafunguka zaidi kiuchumi,”. Rais Samia amesema.

Ameongeza kuwa vituo hivyo vitaongeza ajira kwa vijana ambalo ndo kusudio la serikali kuhakikisha miradi ya kitaifa inanufaisha vijana.





RAIS SAMIA: VIJILI 59 BAHU KUPATA MAJI

Mgombea Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Samia Hassan Suluhu amesema, akipewa ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atahakikisha vijiji vyote 59 vya wilaya ya Bahi vinapata maji.

Rais Samia ameyasema leo alipokuwa anahutubia wananchi waliofika kumsikiliza wilayani Bahi.

“Kati ya vijiji 59, 56 vimepata maji nitahakikisha vyote vinapata maji”. Amesema Rais Samia.

Ametaja vijiji vya Mpamatwa na Ibinwa kuwa ndio vimebaki bila kupata maji ila kazi inaendelea ili kuondokana na adha hiyo.



MRADI WA MAJI KUTOKA ZIWA VICTORIA KUINUFAISHA BAHİ



Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema akipata ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atahakikisha wilaya ya Bahi inafaidika na mradi wa maji kutoka ziwa Victoria.

Rais Samia amesema hayo leo wakati akihutubia wananchi wa wilaya ya Bahi akiwa njiani kuelekea Singida katika kampeini za urais.

“Maji kutoka Victoria yatatumika pia Bahi na hilo ndio kusudio la Kitaifa,” amesema Rais Samia.

Ujenzi wa mradi mkubwa wa maji kutoka ziwa Victoria utaleta suluhisho la kudumu la upatikanaji wa maji safi na salama kwa wilaya ya Bahi.



RAIS SAMIA KUJENGA DARAJA LA MTO NKOGWA WILAYANI BAHİ

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema akipata ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atahakikisha serikali inajenga daraja la mto Nkogwa ambalo limekuwa kero kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo.

Dkt. Samia ameyasema leo wilayani Bahi wakati akihutubia wananchi waliokusanyika kusikiliza akinadi sera zake na za chama.

Amesema usanifu wa daraja hilo ambalo linaunganisha wananchi wanaoishi vitongoji vilivyopo upande wa pili wa kijiji cha Bahi sokoni na yalipo makao makuu ya wilaya ya Bahi umekamilika.





RAIS SAMIA KUJENGA CHUO CHA VETA MANYONI

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Samia Suluhu Hassan ameahidi kujenga chuo cha VETA wilaya ya Manyoni mkoani Singida ili kuwapa vijana ujuzi unaotakiwa waweze kujiajiri na kujikwamua kiuchumi.

Dkt. Samia amesema hayo leo wakati akihutubia wafuasi wa chama hicho waliokusanyika wilayani humo kumsikiliza akinadi sera zake na za chama.

“Tunaenda kujenga chuo cha VETA hapa ili vijana wasome na wapate ujuzi ili waweze kujiajiri na kujiongezea kipato na kuchangia katika uchumi wa taifa,” amesema Dkt. Samia.





Wananchi wa Mpanda Mjini waliofika kwenye Mkutano wa kampeni za CCM wakifurahi pamoja na Mgomba mwenza Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi alipomaliza kuzungumza na kuwasilisha Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na kueleza dhamira ya dhati ya Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuwaletea maendeleo wakazi wa Mpanda Mjini.



Mgomba mwenza Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi wakati akihutubia maelfu ya wakazi wa Mpanda Mjini kwenye mkutano wa kampeni za CCM uliofanyika Mpanda kwa ajili ya kuomba kura za Ndiyo kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.





DKT. NCHIMBI AAHIDI KUBOresha MFUMO WA MAWASILIANO KUTATUA KERO ZA WANANCHI

Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Emmanuel Nchimbi, amesema chama hicho endapo kitapata ridhaa ya kuongoza katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba 29, 2025, kitaboresha mfumo wa mawasiliano nchini.

Amesema hayo leo kwenye kampeni za urais zilizofanyika Viwanja vya Majengo wakati akihutubia wakazi wa Manispaa ya Mji wa Sumbawanga mkoani Rukwa katika kusaka kura kwa mgombea wa CCM, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

“Ndugu wananchi, iwapo mtatupa ridhaa ya kuongoza Taifa letu, ninawaahidi kwamba Serikali yetu ya CCM itaboresha mfumo wa mawasiliano utakaorahisisha kutatua kero mbalimbali za wananchi toka ngazi za chini,” Dkt. Nchimbi anasema.

Dkt. Nchimbi amemaliza ziara ya kufanya kampeni mkoa wa Rukwa leo.



RAIS SAMIA: TUTAJENGA BARABARA YA LAMI KUTOKA MAKONGOROSI-RUNGWA-ITIGI HADI MKIWA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema akipewa ridhaa ya kuongoza tena atahakikisha anakamilisha ujenzi wa barabara ya Makongorosi- Rungwa- Itigi hadi Mkiwa kwa kiwango cha lami ili kukuza biashara kati ya Singida na Mbeya.

Rais Samia ameyasema hayo leo wakati akihutubia maelfu waliokusanyika kumsikiliza akinadi sera zake na za Chama.

“Barabara hii ikikamilika itafungua biashara kubwa kati ya Singida na Mbeya”, Dkt Samia amesema.





RAIS SAMIA KUJENGA DARAJA LA SANZA WILAYA YA MANYONI



Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dkt. Samia amesema iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza tena atahakikisha daraja la Sanza pamoja na barabara za kuingia na kutoka(approach roads) zenye urefu wa kilometa 14 zinajengwa kwa kiwango cha lami.

Dkt. Samia ameyasema hayo leo wilaya ya Manyoni wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wa chama hicho waliokusanyika kumsikiliza.

“Mkandarasi ameishapatikana na usanifu wa daraja hilo na barabara zake umeishakamilika,” Amesema Dkt. Samia.

Daraja hili na barabara hizi ni muhimu kwa uchumi wa wananchi wa Manyoni na maendeleo y taifa kwa ujumla.

RAIS SAMIA KUJENGA VITUO 10 VYA AFYA IKUNGI- SINGIDA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi(CCM), Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza tena atajenga vituo 10 vya afya wilaya ya Ikungi mkoani Singida.

Dkt. Samia ameyasema hayo leo wilayani Ikungi wakati akihutubia wafuasi wa chama hicho waliofika kumsikiliza.

“Nitajenga vituo vitano Ikungi Mashariki na vitano Ikungi Magharibi”, amesema Dkt Samia.





KONA YA ILANI

Kudumisha Demokrasia
na Utawala Bora



RAIS SAMIA KUJENGA KONGANI ZA VIWANDA WILAYA YA IKUNGI

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atajenga kongani za viwanda wilaya ya ikungi

Dkt. Samia amesema hayo eo wakati akihutubia wafuasi wa chama hicho waliofurika wilayani humo kumsikiliza.

“Lengo la kongani hizi ni kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa katika wilaya hii,” Amasema Dkt Samia





RAIS SAMIA: TUTABORESHA USIKIVU WA TBC WILAYA YA MANYONI

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema akipewa ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atahakikisha wilaya ya Manyoni inapata usikivu mzuri wa Matangazo ya TBC.

Dkt. Samia ameyasema hayo leo wilaya ya Manyoni wakati alihutubia wafuasi wa chama hicho waliofurika kumsikiliza

*Kutajengwa kituo cha kurusha matangazo ya TBC Itigi hivyo ujenzi wake ukikamilika Manyoni mtapata usikivu mzuri wa matangazo ya TBC," amesema Dkt. Samia.





RAIS SAMIA KUJENGA BARABARA YA IKUNGI-LONDONI-KILIMATINDE(SORYA) KWA KIWANGO CHA LAMI

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema akipewa ridhaa na kuongoza kipindi kingine atakamilisha ujenzi wa barabara ya Ikungi- Londoni-Kilimatinde(Solya) yenye kilomita 117 kwa kiwango cha lami.

Rais Samia ameyasema leo wilayani Ikungi wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wake waliofurika kumsikiliza akinadi sera zake na za chama.

Dkt. Samia amesema ukamilikaji wa barabara hii utafungua fursa nyingi za kibiashara na kurahisha huduma za usafiri wilayani humo





MGONTO AMEMPONGEZA RAIS SAMIA KWA UTEKELEZAJI WA ILANI KWA ASILIMIA 100

Mgombea ubunge kupitia Chama cha Mapinduzi jimbo la Ikungi Mashariki, Thomas Mgonto, amempongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutekeleza ilani ya chama kwa asilimia 100 katika jimbo hilo.

Amesema hayo leo wakati akihutubia wananchi wa wilaya ya Ikungi mkoa wa Singida katika kampeni za urais.

“Wananchi wetu wana furaha kwa kuwa umetekeleza ilani ya CCM kwa kuwapa umeme katika kila kijiji vyote, maji, na umewajengea Barabara. Hawa wananchi wetu wanaiona tarehe 29.10.2025 iko mbali sana wanatamani wangepiga kura hata leo,” amesema Mgonto.





KIMBISA: UTEKELEZAJI WA MIRADI NDIO SABABU YA UMATI MKUBWA KAMPENI ZA CCM

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Dodoma, Adam Kimbisa, amesema umati mkubwa unaojitokeza kwenye Mikutano ya Kampeni za Chama cha Mapinduzi (CCM) ni kutokana na utekelezaji wa kazi mbalimbali zilizofanywa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuonyesha kwa vitendo imani waliyonayo wananchi kwa Rais wao.

Amesema hayo leo wakati akisalimbia wananchi wa wilaya ya Bahi mkoa wa Dodoma katika mkutano wa kampeni za urais.

“Mhe. Dkt. Samia, umati ambao umekuwa ukijitokeza kukusikiliza kwenye mikutano ya kampeni ya CCM ni kutokana na kazi ambazo umezifanya. Kila mmoja wetu aliyehudhuria hapa hakuna ambaye hajaguswa na kazi ambazo umezifanya,” amesema Kimbisa.





RAIS SAMIA KUJENGA 'MACHINGA COMPLEX' MJINI SINGIDA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema akipewa ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atajenga jengo kubwa na la kisasa la wajasiriamali wadogo almaarufu 'Machinga Complex' mkoani Singida.

Rais Samia ameyasema hayo leo mjini Singida wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wa chama hicho waliofurika kumsikiliza akinadi sera zake na za chama.

"Lengo la soko hili ni kuhakikisha wafanyabiasha wadogo wanafanya biashara zao kwa utulivu na amani ili kukuza uchumi wao na wa taifa," amesema Dkt. Samia.





RAIS SAMIA KUMALIZA KUJENGA SOKO LA KIMATAIFA LA VITUNGUU MKOANI SINGIDA

Mgombea wa urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atahakikisha ujenzi wa soko la kimataifa la vitunguu linalojengwa mkoani Singida linakamilika.

Dkt. Samia amesema hayo leo mjini Singida wakati akihutubia maelfu ya wana CCM waliofurika kumsikiliza akinadi sera za chama hicho.

“Soko hili litafungua fursa kubwa za zao la vitunguu hivyo wafanyabiashara pia mjipange kufungua na kufaidika na fursa hiyo”, amesema Dkt. Samia.





RAIS SAMIA KUTAFUTA SOKO LA MBAAZI NA DENGU NJE YA NCHI

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema akichaguliwa kipindi kingine ataendelea kuwatafutia wakulima soko la kuuza dengu na mbaazi nje ya nchi.

Rais Samia ameyasema hayo leo Mkoani Singida wakati alihutubia wafuasi wa chama hicho walifurika kumsikiliza akiomba ridhaa ya kuchaguliwa tena.

“Serikali itatoa vibali kusafirisha mbaazi na dengu nje iwapo mnunuzi a t a p a t i k a . T u m e a i s h a a n z a mazungumzo na mnunuzi kutoka India,” Amesema Rais Samia.

Ameongeza kuwa mwaka huu mazao hayo yamesitawi kwa wingi duniani hivyo soko lake limeshuka lakini serikali itasimamia kuuza kwa bei ya asilimia 60 ya soko la dunia.





RAIS SAMIA:TUTAJENGA UWANJA MKUBWA WA NDEGE MKOANI SINGIDA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi(CCM) Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema akipewa ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atajenga uwanja mkubwa wa ndege mkoani Singida.

Rais Samia amesema hayo mjini Singida leo wakati akihutubia maelfu ya wananchi wa Singida waliofurika kumsikiliza akinadi sera za chama chake.

“Tukijaaliwa huko mbeleni na hapa Singida tutajenga uwanja mkubwa wa ndege kufungua zaidi fursa za biashara mkoani humu,” amesema Rais Samia.





KEVIN FALLEN



ssh_anatekeleza